

**FAHAMU  
UGONJWA WA  
KICHAA  
CHA MBWA**

**TUSHIRIKIANE  
KUUTOKOMEZA**



## UTANGULIZI

Kichaa cha Mbwa ni ugonjwa hatari, husababishwa na virusi vinavyojulikana kama *Lyssavirus*. Ugonjwa huu huwapata wanyama na binadamu kwa kung'atwa na mnyama mwenye virusi vya ugonjwa. Ugonjwa huu hauna tiba ila unazuilika kwa njia ya chanjo.

### 1. JINSI KICHAHA CHA MBWA KINAVYOENEA

Njia kuu ya kuenea kwa kichaa cha mbwa ni kwa kung'atwa na mbwa au mnyama mwenye virusi vya ugonjwa huu.

### 2. DALILI ZA UGONJWA KWA MBWA

- Kubadilika tabia; kuwa mpole zaidi au mkali zaidi
- Kuogopa maji na mwanga

- Kuhangaika hangaika Kushitukashituka, Kukimbia hovy hovy.
- Kutembea masafa marefu
- Kutokwa mate mengi Kushambulia na kuuma vitu mbalimbali kama vyuma, vijiti, watu, wanyama, n.k.
- Kushindwa kula au kunywa maji
- Kudhoofu, kupooza, na hatimaye kifo.


Kwa wanyama wengine, kama mbuzi, ng'ombe, paka, nguruwe, n.k. dalili hizi na nyinginezo zinaweza kujitokeza kulingana na aina ya wanyama.

### 3. DALILI ZA UGONJWA KWA BINADAMU

- Homa
- Kuumwa kichwa
- Kuchanganyikiwa na kuvunja / piga vitu
- Maumivu ya mwili
- Kuwashwa sehemu ya jeraha
- Kuweweseka, kushtuka mara kwa mara na kuogopa.

- Kuogopa mwanga, upepo au kunywa maji
- Kutokwa na mate mengi mfululizo
- Kupooza, Kudhoofu na hatimaye kifo

#### **4. JINSI YA KUMUHUMIA MTU ALIYEUMWA NA MNYAMA**



Osha jeraha kwa maji mengi yanayotiririka na sabuni

- Safisha kidonda kwa maji mengi yanayotiririka kwa sabuni kwa dakika 10 - 15. (Epuka kutumia mafuta ya taa na dawa nyingine yoyote ya asili kwenye jeraha la kuumwa na mbwa).
- Nenda haraka kwenye kituo cha huduma za afya kilicho karibu ili upate chanjo ya kichaa cha mbwa na pepopunda
- Unapoanza chanjo ya kwanza ya kichaa cha mbwa, hakikisha unapata chanjo zote kadri utakavyoshauriwa na mtoa huduma katika kituo cha afya
- Toa taarifa juu ya mbwa aliyekung'ata au anaye hisiwa kuwa na kichaa kwa mtaalamu wa mifugo ili hatua zichukuliwe haraka kumfua tilia mbwa huyo.



## MAMBO YA KUZINGATIA

Jinsi ya kuzuia kuenea kwa ugonjwa wa kichaa cha mbwa

- Chanja mbwa na paka wako kila mwaka
- Fungia mbwa wako kwenye banda kuanzia saa 12 asubuhi na kumfungulia saa 4 usiku.

**NB: Toa taarifa kwenye Serikali ya Mtaa au Kijiji, Mtaalamu wa Mifugo juu ya mnyama anayehisiwa kuwa na kichaa cha mbwa au mzoga .**



**World Health  
Organization**

Imetayarishwa na Wizara ya Afya na Ustawi  
kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo na Mifugo na Uvuvi.